

LEARNING BY EAR

“The Lost Kid – the Story of Single Mothers in Africa”

EPIISODE 4: “Reality and Fairy Tales”

AUTHOR: Mantegaftot Sileshi Siyoum

EDITOR: Stefanie Duckstein, Adrian Kriesch

PROOFREADER: Kate Hairsine

List of characters by scene:

SCENE ONE: AFTERNOON IN BEGIDU'S TOWN

- **Samy (m, 6)**
- **Begidu (m, 7)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE TWO: AFTERNOON AT MR. KASU'S HOME

- **Papa Telahun (m, 76)**
- **Mama Beletu (f, 65)**
- **Mr.Kasu (m, 60)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE THREE: AT NIGHT IN A LOCAL TAVERN

- **Jonas (m,15)**

- **Mekete (m,16)**
- **Challa (m,17)**
- **Drunkard Minabu (m, 55)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE FOUR: AT NIGHT AT ASKALE’S HOUSE

- **Askale (f,21)**
- **Kassech (f, 22)**
- **Samy (m, 6)**
- **Narrator (m, around 35)**

INTRO:

Hamjambo, wapendwa wasikilizaji! Mnasikiliza mchezo wetu wa redio wa Noa Bongo Jenga Maisha Yako ““MWANA MPOTEVU- KISA CHA KINA MAMA WANAOWALEA WATOTO WAO BILA BABA ZAO BARANI AFRIKA”” “. Leo, tunakuletea sehemu ya nne iitwayo “UKWELI NA HEKAYA”. Mara ya mwisho mlipotutegea sikio, Begidu mwenye umri wa miaka saba na rafiki yake Samy waliokuwa ndio wameshaanza shule walipata matokeo yao ya kwanza ya mwaka. Begidu hakufanya vizuri, jambo lililomuudhi si haba mamake, Kassech. Begidu anaamini kwamba rafiki yake Samy ndiye aliyemjulisha mamake kuhusu matokeo yake mabaya. Begidu ana hasira na anaamua kumuuliza Samy.

SCENE ONE: DAY TIME IN BEGIDU'S SUBURB

1a) SFX: OUTSIDE AMBIENCE, CHILDREN PLAYING

1. **Samy:** Sikumwambia mtu mimi.
2. **Begidu:** Mama yangu alijua vipi?
3. **Samy:** Sijui! Mimi nilimwambia mamangu kuhusu matokeo yangu tu.

KW BEGIN

4. **Begidu:** Muongo wewe!
5. **Samy:** Mimi si muongo! **(Disappointed)**
Usinitukane!
6. **Begidu:** Samahani! Mbona ukamwambia kila mtu kwamba
ninaomba chakula?
7. **Samy:** Sikumwambia mtu yeyote!
8. **Begidu:** **(Aggressive)** Muongo mkubwa! Mjinga wa
mwisho!
9. **Samy:** **(Gets angry)** Hapana, si mimi! Mjinga ni wewe!
10. **Begidu:** Mwanaharamu wewe!
11. **Samy:** Na wewe pia ni mwanaharamu! Lakini afadhali
mamangu kuliko mamako; watu wote wanasema
hivyo! Sijawahi kwenda kudoea chakula kwa mtu!

KW END

12. **Begidu:** Najuwa wewe ndiye uliyemwambia mamangu
matokeo yangu, mpumbavu mkubwa!
13. **Samy:** Mpumbavu ni wewe.
14. **Begidu:** Ebu njoo tuone nani mwanaume! **(Starts fighting.**

Improvise this fight; in postproduction, we can mix it under the narration).

15. **NARRATOR:** Vita kati ya vijana hao wawili vinapamba moto! Watoto wengine wanawazingira na kushangilia. Watoto hao wawili wanaaza kurushiana mawe na Begidu anapigwa kichwani. Begidu anaanza kuvunja damu jambo linalomfanya kuanza kulia; Samy anakimbia mara moja. Wakati huo huo, kwenye eneo jingine, Papa Tilahun na Mama Beletu wamealikwa nyumbani kwa Bwana Kasu, tajiri wa kupigiwa mfano.

SCENE TWO: AFTERNOON AT MR. KASU'S HOME

16. **SFX: RADIO MUSIC IN BACKGROUND**

17. **SFX: CUTLERY ON PLATE**

18. **Papa Tilahun:** Chakula kitamu sana, Bwana Kasu!

19. **Mama Beletu:** Naam, kitamu sana!

20. **Kasu:** Asanteni sana Papa Tilahun na Mama Beletu kwa kuja kwangu leo. Kwa hivyo tufungueni chupa ya mvinyo ili tujadili kadhia yenu hiyo ya dharura; kweli nyinyi hamnywi pombe kali.

21. **Mama Beletu:** Kweli hatunywi.

22. **SFX: OPENING A BOTTLE OF WINE**

23. **SFX: LIQUID BEING POURED INTO GLASSES**
KW BEGIN

24. **SFX: GLASSES CLINKING SOUND**

25. **Kasu:** Kwa afya yenu!

26. **Papa Tilahun:** Na kwa afya ya familia zetu!

27. **Mama Beletu:** Na kwa watoto wetu, pia!

28. **Papa Tilahun: (With emphasis)** Kwa watoto wetu, pia!

29. **Kasu:** **(Not impressed at the same time)** Kwa watoto wetu, pia.

30. **Papa Tilahun:** Muda mrefu sana tangu tulipoonana.

31. **Mama Beletu:** Takribani miaka kumi na mitano.

32. **Kasu:** Naam, wakati wenda mbio!

33. **Papa Tilahun:** Maanake mara ya mwisho tulipoonana ilikuwa miezi michache kabla ya Jonas

kuzaliwa.

KW end

34. Kasu: Vipi hali ya wanangu?

35. Mama Beletu: Naam, Kassech na Jonas wanahitaji
msaada wako kwa dharura – sasa hali yao
imezidi kuzorota.

36. Papa Tilahun: Ndiyo, Ndiposa tumekutembelea hivi leo.

- 37. Kasu:** Nilikia hivyo, lakini tunapaswa kulizungumzia jambo hilo haraka haraka. Mke wangu na mabinti zangu watatu wataingia nyumbani wakati wowote kuanzia sasa.
- 38. Papa Tilahun:** Bwana Kasu, tunafahamu kwamba unajitenga na familia yako ya zamani kwa sababu ya familia yako mpya.
- 39. Mama Beletu:** Tunaelewa na tunaiheshimu familia yako mpya pia.
- 40. Papa Tilahun:** Lakini Jonas na Kassech ni jamaa zako pia.
- 41. Kasu:** **(Inhales deeply and exhales)**
- 42. Mama Beletu:** Sasa hivi wana matatizo makubwa.
- 43. Papa Tilahun:** Walizozana na wakapiga jana usiku hadi ya Jonas kutoroka nyumbani.
- 44. Kasu:** Walikwenda wapi?
- 45. Mama Beletu:** Tumesikia kwamba anaishi nyumbani kwa rafiki yake.

46. Papa Tilahun: Bwana Kasu zingatia hilo jambo sasa hivi. Ukichelewa huenda mambo yakaharibika zaidi. Tafadhali jitoe kimasomaso na uyatwae majukumu ya familia yako ya zamani.

47. Kasu: Siwezi. Kusema kweli siwezi, Papa Tilahun! Wajua nina familia nyingine. Baada ya miaka yote hii iliyopita, nitawatokezea vipi ghafla kisha niwaambie: “Jamani nisikizeni! Mimi nina watoto wengine wawili.” Siwezi kwa kweli! Ndoa yangu itavurugika mara moja bila shaka! Nao Kassech na Jonas hawataamini kwamba mimi ni baba yao wala hawatanikubali!

48. Mama Beletu: Bwana Kasu, hao watoto wanahitaji msaada wako kwa dharura! Yasije kuwa yale yaliyosema kuwa majuto ni mjukuu! Fanya haraka haraka, sasa hivi!

49. SFX: OUTSIDE CAR HORNS

50. Kasu: Hilo ni gari la mke wangu. Haya tutayazungumza wakati mwingine. Yuko wapi huyo mhudumu mvivu? **(angry and speaks to himself)** Yaani nifungue langu mimi mwenyewe!? **(to his guests)** Nisubirini, tafadhali! Narudi hivi punde.

51. Papa Tilahun: Tutasubiri.

52. Kasu: **(While he walks to the door, he calls out**

to the housemaid). Uko wapi wewe?!

Azalu! Azalu!

53. SFX: OUTSIDE CAR HORNS AGAIN

54. NARRATOR: Zamani, Bwana Kasu aliamua kuweka siri kuhusu maisha yake ya awali kwa kuwa hakutaka kuiudhi familia yake mpya. Miaka mingi iliyopita Bwana Kasu aliachana na mkewe wa kwanza na watoto wake, Kassech na Jonas na akamuoia mwanamke tajiri akajaliwa mabinti watatu. Hata Kassech na Jonas hawajui ikiwa Bwana Kasu ndiye baba yao. Bwana Kasu hajui jinsi mwanawe Jonas anavyoenda maisha yake.

SCENE THREE: AT NIGHT IN A LOCAL TAVERN

55. ATMO: MANY PEOPLE IN THE LOCAL BAR

56. SFX: HOMEMADE BIER BEING Poured INTO GLASSES

57. Jonas: **(Happy)** Naam, jamani, ebu tujitumbuize kwa pombe ya kienyeji.

KW Begin

58. Mekete: Umenena, Jonas. Twendeni tukakae pale.

59. Jonas: Hapana! Humwoni yule mlevi wa kutupwa

pale? Minabu, anayeishi nyumba jirani na y a dada yangu.

60. **Challa:** Tukae karibu naye basi. Jamaa mwenyewe anachekesha, halafu huenda akatununulia kinywaji.

61. **Mekete:** Challa, hatujaja hapa kuchekeshwa.

62. **Minabu:** **(He is a bit drunk, and calls out the boys from a distance)** Nyinyi! Vijana! Njoooni hapa!

63. **SFX: GLASS BEING PUT HARSHLY ON THE BENCH**

64. **Minabu:** Nimesema, njoooni hapa, nyinyi vijana watu! **(Laughs)**. Najua mnatoka kitongojini kwangu.

65. **Challa:** **(To Minabu)** Ebu kunywa pombe yako unayokunywa!

66. **Minabu:** Ati! **(Pause)** Haya, Haya! **(laughs)** Sawa! Ikiwa hamtaki kuja hapa nilipo, hakuna shida, nitawauliza swali kutokea hapa. **(laughs)** Mnafanya nini kwenye baa hii badala ya kwenda shuleni?

67. Challa: **(Mocking at him)** Bwana Minabu,
Tumekuja hapa kukununulia kinywaji!

68. Minabu: Kuninunulia kinywaji? **(Laughs)**.

69. Jonas: Jamaa! Achaneni na huyo mlevi, bora tukae
hapa.

70. ATMO: MANY PEOPLE IN THE LOCAL BAR

71. Minabu: **(Continues speaking from a distance)**.

KW Ende

72. Three teenagers: **(Speaking in a low voice)**.

73. Mekete: Kwa hivyo ulisema wana mbwa mkali sana.

74. Jonas: Naam, tatizo kubwa hilo.

75. Mekete: Hapa, si tatizo kubwa. Tunaweza kumrushia
mbwa huyo nyama yenye sumu.

76. Challa: Naam!

77. Jonas: Tukifanya hivyo, tunaweza kuuruka wigo
bila shida.

78. **Challa:** Naam, tunaweza kufanya hivyo! Jina lake nani?

79. **Jonas:** Jina la nani?

80. **Challa:** Huyo mtu mwenye mbwa mkali (**Laughs sarcastically**).

81. **Jonas:** Ewe kijana! Wewe ni msahaulifu mno. Jina lake ni Kasu. Bado hujaanza kunywa pombe na umeshasahau jina lake.

82. **Challa:** Ndiyo, ndiyo, Bwana Kasu.

83. **Mekete:** Basi, tuanzeni kunywa kwa ajili ya Bwana Kasu (**Laughs**).

84. **Jonas:** Kwa ajili ya Bwana Kasu!

85. **Challa:** Yuko wapi huyo mhudumu? (**calls out**)
Ebu! Njoo. (**Claps his hands**) Njoo!

86. **NARRATOR:** Mambo yamechacha! Mwana hajui kwamba anatunga njama ya kumwimbia baba yake mzazi. Tuachane na Jonas na wenzake kwenye baa na twende nyumbani kwa Askale. Hana habari kuhusu vita kati ya mwanawe na Begidu. Hapo alipo anamkumbatia mwanawe wala hajui yaliyotukia.

SCENE FOUR: AT NIGHT AT ASKALE’S HOUSE

87. SFX: NIGHT AMBIENCE

88. Askale: Basi, mwanangu Samy, leo nitakusimulia hadithi kuhusu “Fisi mjinga mlafi na nyani mwerevu”..

89. Samy: **(Happily)** Haya, ma, niambie.

90. Askale: Vyema! Hapo zamani za kale, kuliwepo fisi mjinga na mlafi na nyani mwerevu .

91. Samy: Sa..wa!

KW Beginn

92. Askale: Jua liliendelea kutoka taratibu huku likitoa

miale miekundu. Nyani alikuwa akiirukia miti, Ghafla alitazama chini akamuona fisi mpumbavu na mlafi akikimbia kupitia shambani akielekea pango mwake. Alitaka kufika kwenye pango lake lenye kiza kabla ya jua kutoka kabisa. Nyani alicheka kwa sauti kubwa alipomwona fisi jinsi alivyokuwa akikimbia. Fisi alimtazama nyani kwa hasira kisha akiendelea na mbio zake. Nyani alicheka tena. Siku iliyofuata...
(interrupts her tale).

KW Ende

93. **SFX: DOOR KNOCKED HARSHLY**

94. **Askale:** **(Surprised)** Nani huyo?!

95. **SFX: DOOR OPENED**

96. **Kassech:** **(Very angry)** Ndiyo, unakaa kumkumbatia mwanao mwenye adabu, ilhali mwanangu anavuja damu kichwani!

97. **Askale:** Kuna nini, Kwani Begidu amepatikana na nini?

98. **Kassech:** **(Warns her)** Vyema na wewe

ukashughulika zaidi kumlea MTOTO
WAKO kwa njia ifaayo, kuliko kuniambia
MIMI kila mara kwamba nimzingatie zaidi
mtoto WANGU.

99. **Askale:** Sielewi unachokizungumzia. Kassech,
tafadhali keti. Kwani kuna shida?

100. **Kassech:** **(Repeating Askale's words)** Kwani kuna
shida? **(Laughs angrily and leaves).**

101. **SFX: DOOR SLAMS**

102. **Askale:** **(Upset)** Kwani umemfanya nini Begidu?

103. **Samy:** Yeye ndiye aliyeanzisha vita.

104. **Askale:** Ati! Kwa nini mlipigana? Ebu niambie!
Ulimfanya nini?

105. **Samy:** **(Scared)** Alianza kunirushia mawe.

106. **Askale:** Na kisha, ukampiga kichwani?

107. **Samy:** Sikuwa na nia ya kumpiga kichwani.

108. **Askale:** Je ni sawa kurusha mawe?!

109. **Samy:** Hapana, ma. **(Starts crying).**

110.Askale: Sawa! Leo hapana cha “Fisi na nyani” au hadithi nyingine yoyote. Nenda kalale!

111.Samy: Ma...

112.Askale: Nimesema, nenda kalale! Haya tutayazungma kesho asubuhi.

113.Samy: **(Goes to his bed).**

114.SFX: NIGHT AMBIENCE

OUTRO:

Usiku huo, Begidu anatoweka nyumbani kwa mara ya pili. Mwanzoni mama yake Kassech anafikiri kwamba anajificha nyumbani kwa Papa Tilahun, lakini hayupo. Inaonekana kana kwamba Begidu ameondoka nyumbani kabisa kama alivyofanya Jonas, mjombake. Lakini Begidu yuko wapi? Utajua hayo katika sehemu itakayofuta. Kumbuka unaweza kusikiliza sehemu hii na sehemu nyinginezo katika ukurasa wetu wa tovuti, dw.de/lbe. Tukutane kwenye sehemu inayofuata- Kwaheri!